**BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU KIDATO VI**

**KISWAHILI 1**

**( Kwa Watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)**

**121/1**

**MUDA: SAA 3** **Jumanne, 4 Machi 2025 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali nane (8.
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali matatu (3) kutoka sehemu B. Swali **la nane (8)** ni la lazima.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata:-

Ilikuwa usiku wa manane, siku nisiyoweza kuisahau, usingizi ulinipaa, mawazo yakaingia kichwani mwangu. Nje kulikuwa na giza nene lililotanda angani. Kwa mbali, nilisikia bundi wakilia na wadudu wakitoa milio inayovutia. Macho yangu yakielekea juu ingawa hakuna nilichokiona.

Nilizama katika dimbwi la Mawazo kiasi cha kuhama nilipokuwa. Ooh! Masikini, kwanini hakusikiliza ushauri? Ama kweli asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Mh! Lakini kwanini? Anhaaa! Wahenga walisema, "mkataa pema pabaya panamwita." Dimbwi hili la mawazo liliwahusu Machupa na Dimoso, vijana waliokuwa maarufu katika Kijiji chetu. Vijana hawa walikuwa viongozi wa wanafunzi katika shule ya sekondari Mshikamano.

Baada ya kuhitimu kidato cha sita, Dimoso alifaulu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro. Yeye alisomea Afisa Mwajiri. Machupa alichaguliwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kusomea shahada ya Uhasibu. Wanakijiji walifurahi sana. Tulikuwa na matarajio makubwa kwa wasomi hawa.

Siku moja majira ya asubuhi nilipata fununu iliyokuwa ikisambaa kijijini kumuhusu Machupa. Moyo ulienda mbio na macho ya wengi yalibaki yakitiririka machozi na kukodolewa. Ooh! Masikini Machupa! Mzee mmoja alisikika. Kumbe alipofika chuoni, alijiunga na makundi ya vijana wa mtaani waliotumia mihadarati. Ni mwaka mmoja sasa umepita tangu alipojiunga na Chuo, sasa akili zimemruka amekuwa kama teja! Hawezi tena kusoma.

Wazazi wake walimpeleka hospitali ya Taifa Muhimbili kupatiwa matibabu, lakini bado hali haikuwa nzuri.

Mihadarati ilimuathiri sana na hata kupelekea kuwa mkorofi sana na kupigana na watu mara kwa mara mpaka kujeruhiwa kichwani na kuathiri ubongo wake. Ndoto zake zote zimepotea. Wazazi na jamii tumepoteza nguvu ya Taifa. Alishauriwa sana aachane na vikundi hivyo lakini hakusikia, hakika mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idi. Ghafla nilianza kusinzia kwa huzuni ya moyo na kutokomea katika ulimwengu wa njozi.

**MASWALI:**

(a) Andika kichwa cha Habari kinachofaa kwa habari hii uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi matano.

(b) Toa methali moja kwa kila methali zilizotumika katika habari uliyosoma
   (i) Mkataa pema pabaya panamwita
   (ii) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
   (iii) Mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idi.

(c) Je, unadhani ni kwanini vijana wengi siku hizi hujikuta wakitumbukia kwenye dimbwi hili la utumiaji wa mihadarati uliokithiri? (Toa hoja mbili).

(d) Ukiachana na athari za utumiaji wa mihadarati zilizoelezwa katika habari hii, Je, ni zipi athari nyingine zinazowakabili vijana waliojiingiza katika sakata hili? (Toa hoja mbili).

(e) Ukiwa kama raia mwema, Je, utaisaidia vipi serikali kupigana vita na hili sakata la vijana wadogo kujiingiza katika wimbi la utumiaji wa mihadarati linalokithiri siku hadi siku? (Toa hoja mbili)

2. "Mtazamo wa kimofolojia ulioasisiwa na akina Broomfield 1935, Guthrie 1948 na Palome 1967 ndio msingi mkuu wa kuainisha ngeli za nomino za Kiswahili. Licha ya umuhimu wake huo, pia ulikuwa na madhaifu yake." Thibitisha kauli hiyo kwa kutumia hoja tano (5).

3. "Kirai Nomino (KN), kimeundwa na miundo tofauti tofauti ili kumtimizia mtumiaji wa lugha lengo la mawasiliano." Jadili usemi huu kwa kutumia hoja tano (5) na mifano kuntu.

4. Ili kuikuza lugha na kuipamba pia, watumiaji wa lugha nyingi hujikuta wakiangukia kwenye matumizi ya misimu katika maisha yao ya kila siku. Aghalabu matumizi hayo huwa na changamoto mbalimbali katika lugha. Ukiwa kama Mkufunzi wa lugha ya Kiswahili eleza changamoto hizo kwa mifano kuntu. (Toa hoja tano (5)).

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **nane (8)** ni la **lazima**

5. "Ili kirahisisha baadhi ya mambo katika jamii, matangazo yana nafasi kubwa sana." Thibitisha kauli hii kwa kujibu maswali yafuatayo:
   (a) Je, tangazo ili liwe bora linapaswa kuwa na sifa zipi? (Toa hoja tano)
   (b) Ukiwa kama Mkurugenzi wa TAASISI YA MOYO YA JAKAYA KIKWETE (MUHIMBILI), andika tangazo kuuarifu umma juu ya zoezi la kujitolea kutoa damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa waliofanyiwa operesheni kwenye taasisi hiyo. Zoezi hilo litafanyika siku ya Jumamosi ya tarehe 07/03/2025 katika viwanja vya Hospitali ya Taifa Muhimbili, kuanzia majira ya saa tatu asubuhi mpaka saa kumi alasiri.

6. "Kabla ya Tanganyika kupata uhuru chini ya utawala wa Muingereza, mashirika mengi ya Wamisionari kama vile CMS, UMCA an S.P.C.K yakiongozwa na Maaskofu wao kama vile Edward Steer, A. Madan na F. Johnson, yalitoa mchango mkubwa katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja sita.

7. Ni kweli usiopingika kwamba ili kupiga hatua maishani kutoka hali fulani ya kimaisha kwenda hali nyingine ni lazima ukutane na changamoto mbalimbali kama ilivyo kwa lugha ya Kiswahili ambayo imekuwa ikitanua mbawa zake kimataifa licha ya kukutana na changamoto kedekede. Jadili changamoto hizo kwa mifano maridhawa. (Toa hoja tano (5)).

8. Bwana Makame ni Mkufunzi katika Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Wakati wa ufundishaji wa kazi ya tafsiri na ukalimani, alidadavua kinagaubaga zana muhimu za kuzingatia wakati wa ukalimani. Je, unadhani ni zana zipi bwana Makame alizidadavua? (Toa hoja tano (5)).

*Wabillah Tawfiiq*